# MKATABA WA MAUZO YA ARDHI

## KATI YA

## FAIZ IDDI FAIZ na PATRICK MARCUS PUNDA Kama wasimamizi wa Mirathi ya Marehemu MARCUS PUNDA (kwa niaba ya warithi wote wa MARCUS PUNDA)

## NA

## MOYO AFRICA EXPLORATIONS LIMITED

---

KWA MAUZO YA ENEO LILILOPO PWANI YA MBUTU,
MTAA WA MBUTU – MKWAJUNI KATA YA SOMANGILA
WILAYA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM

---

**IMETENGENEZWA NA:-**

WAKILI
JUMA NYAMUGARURI
P. O. BOX 159
DAR ES SALAAM

10 Acre

# MKATABA WA MAUZO YA ARDHI

MKATABA huu umefanyika leo **tarehe** ......16....... **mwezi Julai, mwaka 2009**

KATI ya

**Bw. PATRICK MARCUS PUNDA na Bw. FAIZ IDDI FAIZ ambao ni wasimamizi halali wa mirathi ya Marehemu MARCUS PUNDA (kwa niaba ya warithi wote wa MARCUS PUNDA,** wote wakazi wa Kigamboni – Temeke Dar es Salaam, kwa upande mmoja (ambao katika mkataba huu wataitwa "**WAUZAJI**"),

NA

Kampuni ya **MOYO AFRICA EXPLORATIONS LIMITED** wa Sanduku la Posta 20787, DAR ES SALAAM (ambayo katika mkataba huu itaitwa "**MNUNUZI**").

MKATABA huu **unashuhudia na kuthibitisha** kama ifuatavyo:

1. KWAMBA Wauzaji ni wasimamimizi wa mirathi ya marehemu **Marcus Punda** ambaye ni mmiliki halali wa ardhi inayouzwa ambayo ipo katika Pwani ya Mbutu, Mtaa wa Mbutu Mkwajuni, katika kata ya Somangila, ambayo imetambuliwa na kuonyeshwa kwa Mnunuzi na mipaka yake yote mbele ya mashahidi waliotajwa hapo chini na kuweka saini zao katika hati hii kama ilivyoonyeshwa hapo chini.

   Kwa ufafanuzi zaidi, shamba hili ni la Ekari Kumi (10). Eneo hili limepakana na maeneo jirani kama ifuatavyo:

   **Kusini** : Eneo linalomilikiwa na: MR. TWISHA

   **Kaskazini** : Eneo linalomilikiwa na: UKOO WA MARCUS PUNDA

   **Mashariki** : **Moyo Africa**/Bahari ya Hindi

   **Magharibi** : Mashamba ya Ukoo wa Marcus Punda na nyumba ya mtoto wa Marcus Punda

   Jina: SYLVESTER MARCUS PUNDA (EVARESTO)

2. KWAMBA Wauzaji wakiwa na akili timamu, kwa hiari yao na kwa niaba ya Ukoo mzima na warithi wote wa **Marcus Punda** wanamuuzia Mnunuzi ardhi hiyo ya ekari kumi kwa bei ya SHILINGI MILIONI THELATHINI NA TANO PESA TASLIMU (Shs. 35,000,000/=).

   Mnunuzi atalipa pesa hizo kwa awamu MOJA, ambayo italipwa siku ya kuweka saini mkataba huu na inakubaliwa kuwa Wauzaji kwa kuweka saini zao kwenye mkataba huu wanakiri kupokea fedha hizo zote kama malipo halali na yaliyojitosheleza kabisa. Hakutakuwa na madai yoyote mengine kutoka kwa Wauzaji kwa Mnunuzi.

3. KWAMBA Wauzaji wanauza ardhi hiyo ikiwa haina migogoro yoyote na haiko chini ya madai yoyote ya kifamilia au vinginevyo na kwamba umiliki wa Wauzaji wa ardhi hiyo haugombaniwi wala kubishaniwa na mtu yoyote.

4. KWAMBA endapo Mnunuzi atapoteza umiliki wa ardhi hiyo kutokana na Wauzaji kutokuwa na umiliki halali na thabiti au ardhi hiyo kuwa na mgogoro au migogoro ya umiliki inayowahusisha au kuwahusu Wauzaji kwa jinsi yoyote ile, basi Wauzaji watalazimika kumlipa Mnunuzi pesa zake zote alizolipa ili kununua ardhi hiyo pamoja na riba na gharama ambazo Mnunuzi atakuwa ameingia kutokana na mgogoro au migogoro hiyo na pia malipo ya maendelezo ambayo Mnunuzi atakuwa amefanya katika eneo hilo.

   PIA Wauzaji wataweza kushtakiwa kisheria kwa kosa la udanganyifu pamoja na makosa mengine ya jinai.

5. KWAMBA kwa mkataba huu Wauzaji wanamkabidhi Mnunuzi ardhi hiyo iwe katika milki yake moja kwa moja na hawataingilia kwa namna yoyote ile umiliki wa Mnunuzi.

6. KWAMBA Wauzaji wanatamka kwamba hawajapokea taarifa yoyote kuhusiana na ardhi inayouzwa kuwa katika mpango wowote wa serikali na kuwa hawajapokea taarifa ya kuchukuliwa eneo hilo wala taarifa za fidia kwa ajili ya eneo hilo.

7. KWAMBA Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na Mtendaji wa Kitogoji hawana kipingamizi lolote kuhusiana na mauzo ya eneo au mkataba huu na Wauzaji watawasilisha uthibitisho huo.

8. KWAMBA Wauzaji wanaahidi kushirikiana na Mnunuzi kwa kutoa msaada kumwezesha Mnunuzi kuhamisha umiliki ya ardhi hiyo kisheria kutoka kwa Wauzaji kwenda kwa Mnunuzi.

9. KWAMBA maneno "Wauzaji" na "Mnunuzi" yatahusu na kujumuisha familia, jamii, warithi na wategemezi wa kila mmoja wao kwa madhumuni ya mkataba huu.

**KWA USHUHUDA** na **UTHIBITISHO**, mkataba huu umewekwa sahihi na Wauzaji na Mnunuzi mbele ya mashahidi kama inavyoonyeshwa hapa chini:

IMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA )
na **Bw. Patrick Marcus Punda** )
leo hii tarehe 16 mwezi 07 mwaka )
2009 )

..................................
**MUUZAJI**

Mbele ya:

**WAKILI:**

Saini: ..................................

Ndurumah Keya Majembe (Advocate)
Notary Public & Commissioner for Oaths
P.O. Box 13148 - Dar es Salaam

IMETIWA SAHIHI na KUTOLEWA )
na **Bw. FAIZ IDD FAIZ** )
leo hii tarehe 16 mwezi 07..... mwaka)
2009 )

..........................................
**MUUZAJI**

Mbele ya:

**WAKILI**

Saini: ..........................................

Ndurumah Keya Majembe (Advocate)
Notary Public & Commissioner for Oaths
P.O. Box 13148 - Dar es Salaam

Muhuri:

Wauzaji waliotajwa hapo juu na kutia saini zao mkataba huu, wanafanya hivyo kama Wasimamizi halali wa Mirahi ya Marehemu Marcus Punda na **kwa niaba ya Warithi wote** wa maqli za marehemu Marcus Punda:

1. **ALBERTO MARCUS PUNDA**
   Saini: ..................................  Dole Gumba:

2. **SYLVESTER MARCUS PUNDA**
   Saini: ..................................  Dole Gumba:

3. **CONRAD MARCUS PUNDA**
   Saini: ..................................  Dole Gumba:


4. **LAURENCE MARCUS PUNDA**
   Saini: ..................................  Dole Gumba:

5. **BERNADETHA MARCUS PUNDA**
   Saini: ..................................  Dole Gumba:

6. **HELENA MARCUS PUNDA**
   Saini: ..................................  Dole Gumba:

7. **ODILIO MARCUS PUNDA**
   Saini: ..................................  Dole Gumba:

## SKETCH OF PLOT Nos............. BLOCK ............. AT MBUTU
## KIGAMBONI MUNICIPAL COUNCIL DAR ES SALAAM CITY




SCALE 1:1,500

MP FILE..........................

STD No..........................

COMPS..........................

PLAN No..........................

AMMENDMENTS MADE BY:

1.............................................
2.............................................
3.............................................

PHOTOSTAT COPIES SENT TO:

1.............................................
2.............................................
3.............................................

Plan Drawn by NGONGO,DADI

I hereby certify that the survey represented by this plan was carried out in accordance with the survey regulations.

DATE.........../.........../2020

.............................................

LICENSED LAND SURVEYOR

REGISTERED PLAN No.......................